**[R5652 + R4789]**

# UMUHIMU WA KUJIDHIBITI

**JIJI BILA UKUTA**
**"Asiyejitawala roho yake ni kama mji**
**uliyobomolewa na usio na kuta. "- Met. 25:28.**

*Methali 25:28 TPT Ikiwa unaishi bila kujizuia na hauwezi kudhibiti hasira yako, wewe ni dhaifu kama mji ulio na kinga iliyovunjika, iliyo wazi kushambulia.*

Mfano huu unaopatikana katika maandiko yetu ni yenye NGUVU kweli. Mjini, hasa katika nyakati za zamani, kulikuwa ni mahali ambapo watu walikuwa wanakusanyika ili kujinufaisha na kulindwa. Wanyang'anyi walikuwa nje ya mji tayari kupora ila kuta za mji ziliwahifadhi kutoka kwa madhara hayo, ili wakaazi waweze kulinda vitu vyao vya thamani, haki zao, na maslahi yao.

—

Jiji lolote lenye kuta zilizobomoka lingekuwa na sababu kubwa ya kuwaogopa waporaji kama hao. Lingekaribisha shambulio na kuwa na hakika ya kukutana na maafa wakati fulani.

Kwa kusudi kama hilo, Mungu, katika kumuumba mwanadamu, alimpa *nia*. Ni mojawapo ya vitu vinavyofananisha mwanadamu na Muumba wake. Tunaweza kuwa na nia, hata miili yetu iwe dhaifu, au, hata shauku zetu ziwe na nguvu. Nia hiyo inaweza kuwa na nguvu hata ikiwa tutawekwa chini ya wengine au la**. Miili yetu inaweza kufanywa watumwa, ila nia zetu haziwezi kufanywa watumwa bila ruhusa yetu. Nia yetu ni kitu ambacho hakiwezi kuchukuliwa kutoka kwetu; lakini inahitaji kutetewa; inahitaji kurekebishwa; inahitaji kuimarishwa katika maeneo dhaifu.**

*(John Gill: **Yeye asiyedhibiti roho yake mwenyewe**, .... Nia yake na matamanio yake, hayazuii, kwao, kama neno linavyoashiria; hakuna mlinzi wa kuyalinda, hakuna ua wa kuyazingira, ili kuzuia udadisi wake, kuangalia kiburi chake na ubatili, kuzuia gadhabu yake na hasira na kisasi, na kuweka ndani ya mipaka inayofaa tamaa yake na kuwashwa kwa kujisifu;*

***ni kama mji uliobomoka na bila kuta;** ambamo wanaweza kwenda kwa raha, na ambayo iki wazi kwa unyanganyi na vurugu za kila awaye yule; hivyo ndivyo alivyo yule asiyejidhibiti na kudhitibi moyo wake, kwa kuiacha ikamtawale, huwa wazi kwa adui wa nafsi, yaani Shetani na anakabiliwa na kila aina ya dhambi, mtego na majaribu.)*

Mtu huyu hapa amefananisha mji kama hilo na nia ya kibinadamu iliyovunjika. **Nia daima inastahili kulinda akili na kutoruhusu chochote kiingie hapo isipokuwa kupitia malango yake ya kawaida-yaani Dhamiri na Hukumu. Malango haya yanapaswa kutazamwa kwa ukaribu sana ili yaweze kukubali tu mawazo ambayo hayatasababisha jeraha, yenye manufaa , yenye busara — sawa na Neno la Mungu.**

**Kila mwanadamu anapaswa kuwa na nia na anapaswa kuitunza vyema, anapaswa kuhakikisha kwamba haivunjiki; vinginevyo upotovu wa tabia utafuata**

**HAJA YA KUIMARISHA NIA**

Wale ambao hawazingatii hii na wasioimarisha nia ambapo wanapata dhima maalum ya shambulio, wana hakika ya kuifanya ikavunjike zaidi ili kwamba, pole pole, wafikie mahali ambapo hawana nia kabisa, wakose kujizuia . Kama tu katika mji ulioharibiwa kuta za ulinzi wake zimeharibiwa na adui anapata kuifikia kwa urahisi, **ndivyo mwanadamu anayejitolea kwa dhambi na udhaifu mbalimbali na mashambulio ya Adui amekwishapoteza uanaume wake halisi na yuko katika hatari ya kupoteza kila kitu.**

Ni sehemu ya jukumu letu kama Wakristo na kama Viumbe Vipya kustahimili mashambulio yote ya Adui; na mashambulio haya hayatoki kwa nguvu zinazoonekana peke yake, bali hutoka kwa roho mbaya; hutoka kwa wale ambao wanatafuta kutumiliki-kama ilivyo kwa wale ambao wanadhibitiwa na pepo hawa wabaya. Nia zao zimeshindwa, zimevunjwa, nao wako mikononi mwa maadui zao, hasa kama ilivyoonyeshwa kwenye andiko letu. Wacha nao wajitahidi kumwondoa adui, kumpinga, kuimarisha kuta za akili zao na kufanya ushirika mara moja na Bwana Yesu. Wacha wakampe mioyo yao kikamilifu na kabisa na wakubali nia yake, Neno lake, mwongozo wake, katika kila jambo.

Ni kweli, wanapofunguliwa hivyo kutoka kwenye utumwa wa dhambi na Shetani, wanakuwa watumwa wa haki na wa Kristo; lakini inapogundulika kwamba kuwa watumwa wa Kristo inamaanisha kutumikia kilicho chema na cha kweli na haki, na ni kuwa katika uwiyano na Baba, **wote wanapaswa kufurahi kujiweka kikamilifu na bila kizuizi chini ya udhibiti wa yeye ambaye amependa sana jamii yote ya wanadamu hata kuinunua kwa damu yake ya thamani. Hakika wote wako salama mikononi mwake!**

Lakini haitoshi kwamba yeyote kati yetu ajiweke tu mikononi mwa Bwana. Mtunga Zaburi anatushauri, "Mkabidhi Bwana njia yako; *mtumaini yeye*, naye ataitimiza; naye atatoa haki yako kama nuru." ***Zab. 37: 5.***) Mtume Paulo anatuambia kwamba "Mungu ndiye atendaye kazi ndani yenu, kutaka na kufanya kwa nia yake mema." (***Flp. 2:13.***) Yeye hufanya kazi kupitia ahadi zilizo katika Neno Lake; kupitia uzoefu anuwai wa maisha, nidhamu na michakato ya unyenyekevu, **na ni vyema tuzingatie kila somo kwani huja tunapotaka kuwa na tabia iliyoendelezwa kwa mfano wa Kichwa chetu.**

Nia haimaanishi matamanio hasa. Kuna tofauti kati ya matamanio na nia. Wengine wanatamani kwamba wangekuwa na dola milioni moja, lakini hawana nia hata ya kujaribu kuipata. Wengine wana hamu ya kuamka saa moja asubuhi; lakini hamu hio haiwaamshi, kwa sababu nia imevunjika. Wanajisemea, "Lo, kulala kidogo, kulala kidogo, kukunja mikono kidogo usingizini!" **(Mithali 6:10; 24:33)** Hawana udhibiti wao wenyewe. Wanaweza kudhani watapata udhibiti huu kwa kuweka saa ya kengele. Ila muda kwa muda saa hio ya kengele haiwafaidi tena; hawasikii kabisa.

Yeyote anayeruhusu nia yake kuvunjika atakapopoamka asubuhi atakuwa na nia dhaifu au hata kidogo katika mambo yote. Tunapaswa kutengeneza kanuni njema kwa wakati wetu wa kuinuka

na wa kustaafu. **Kwa kutumia maamuzi yetu bora zaidi juu ya kile kinachopaswa kufanywa, tunafaa kuhakikisha kwamba kimefanywa.** Iwapo jambo hilo halina madhara kwetu au kwa mtu mwingine, basi linapaswa kutekelezwa.

Ni muhimu kutekeleza maagizo ya maamuzi yetu mema ili nia iweze kuimarika, ndiposa mtu huyo asiwe ni wa kuyumbayumba.

Kutokuamua na ukosefu wa tabia katika mabo madogo madogo huathiri mambo yote makubwa maishani. Mtu anayeinuka kwa njia isiyo ya kawaida anaweza kuwa asiye wa kawaida katika biashara. Mtu ambaye hawezi kuamua ni nini anapaswa kula anaweza kuwa hana mpango maishani, ni mlegefu katika maamuzi yake yote. Mtu kama huyo ataweza kuruhusu muuzaji fulani amshawishi juu ya kile atakachonunua. Wengine kwa kiwango kikubwa wako chini ya udhibiti wa wengine.

*(MacLaren: Hapa tuko katika hali ya vita ambayo inahitaji kuwafungia nje maadui kila wakati. Majaribu yapo kila mahali; adui zetu hutuzunguka kama nyuki; uovu wa aina nyingi huvutia. Tunaweza kujiona kama kundi ndogo tu cha maaskari wanaolinda lango dhidi ya majangili wanaojificha tayari kutushambulia iwapo tutalegeza umakinifu wetu kwa muda mfupi tu. Na hiyo ndiyo picha halisi ya asili ya mwanadamu kama ilivyo kuliko ile ambayo watu wengi hudanganywa nayo. Maisha sio uwanja wa michezo, lakini uwanja wa mapambano mabaya, ya jitihada. Hakuna mtu anayefanya vyema katika usingizi wake; hakuna mtu anayefaulu bila mapambano.)*

## "ANAYE TAWALA ROHO YAKE MWENYEWE NI HODARI KULIKO ANAYETEKA MJI "

Hatupaswi kupoteza ukweli kwamba tunapaswa kuwa "wafanyikazi pamoja na Mungu" katika kufanikisha kazi kubwa ya kubadilisha inayofanywa ndani yetu kwa kufanywa upya akili zetu. Vita vyetu dhidi ya *nafsi* ndiyo mapambano yetu kuu zaidi, na tunayo Neno la Bwana kwa ajili yayo kwamba yeye "anayetawala roho yake mwenyewe [nia yake mwenyewe, mawazo yake] ni bora kuliko yule anayeteka mji," kwa sababu amejifunza kwa kiwango hicho kudhihirisha tabia ya kweli katika mwelekeo sahihi-ule wa kujidhibiti.
Ila, tusijekufa moyo kwa mwendo wa pole wa maendeleo yetu, daima tunapaswa kukumbuka kuwa kufikia udhibiti wa nafsi zetu, akili zetu, kuletwa kwa umoja kamili, maelewano kamili, na Bwana na, hadi sasa inavyowezekana, kulingana na watu wote wa Bwana ambao wako sawa naye, inafikiwa "mwishowe," kama vile Mtume anatuarifu; hatua kwa hatua hufikiwa na "kuendelea kwa uvumilivu katika kufanya vyema," kutegemea uhakikisho wa Kiungu wa neema ya kusaidia katika kila wakati wa hitaji.

Wacha sote tuelekeze kila nguvu katika maendeleo haya ya mwisho na makubwa. **Tunapaswa kuwa nayo daima mbele yetu kama kigezo, bora zaidi, lengo, na ingawa tunaweza kushindwa mara kwa mara, ikiwa tunatumiwa sawa katika jambo hilo tutakuwa na nguvu kama matokeo ya kila kutofaulu; kwa kila kutofaulu kutatuonyesha, wazi zaidi kuliko vile tulivyotambua hapo awali, maeneo dhaifu katika tabia zetu**, asili inayotokana na anguko. Na ikiwa kila sehemu dhaifu itaangaliwa kwa uangalifu na kulindwa dhidi ya habari ya siku za usoni, tutakuja, na, kwa neema ya Mungu na chini ya mwongozo wa Mwalimu wetu mkuu, kwa

Neno lake na mfano wake na uongozi wake, katika hiyo hali ya kushinda, hali inayowiyana, ambayo itakubaliana kabisa na mapenzi ya Mungu.

**Kwa waliohivyo, kutazama nyuma, hata makosa ambayo, baadaye yalitambuliwa, yalisababisha kuimarishwa zaidi dhidi ya hila za Adui na udhaifu wa mwili, inaweza kuonekana kuwa imeshindwa na Bwana kwa baraka zetu, kulingana na ahadi yake kwamba "vitu vyote hufanyika kwa wema ya wale wampendao Mungu." - Rom. 8:28.**

---

**Mungu anatafuta tabaka la watu ambao wanatawala *vyema* akili zao**. Ikiwa watajifunza kutawala akili zao kabla ya kuja katika familia ya Mungu, itakuwa bora kwao. Lakini kwa kiwango chochote, njia pekee ambayo wanaweza kuingia katika Ufalme itakuwa kwa kukuza tabia.
Biblia inatuambia hasa ni yapi yaliyo ya mwili, na ni yapi yaliyo ya Roho Mtakatifu, akili takatifu, ya Mungu; ni vitu gani, hasa, vinavyounda tabia takatifu ambayo tunapaswa kuwa nayo. Inatuambia kwamba tunapaswa kuweka mbali hasira, uovu, chuki, uchungu, ghadhabu, hasira, ugomvi; na kwamba tuvae upole, utu wema, uvumilivu, ustahimilivu, fadhila za kindugu, upendo. Masomo haya lazima yafunzwe. Hatuwezi kusema kwamba *mwili* utadhibitiwa kikamilifu; lakini *nia* lazima iwepo, na udhibiti wa mwili kadri inavyowezekana kwa msaada wa Kiungu unapaswa kuendelezwa siku kwa siku.

Bwana anatafuta watu wenye nia imara, tabia dhabiti. Kwa hivyo lazima kuwe na mabadiliko chanya kwa Bwana na agano dhahiri na Yeye mwanzoni, la sivyo hatukubaliki kwa Baba. Halafu baada ya kuja katika familia Yake tunapata kuwa vitu kadhaa ambavyo tulifikiri kuwa *ni sawa* na ya*sio saswa* lazima virekebishwe; na kwa kadiri tulivyokuwa katika maisha yetu ya zamani tulitawala akili zetu wenyewe, tukadhibiti hamu zetu za mwili na misukumo, vivyo hivyo tutafanya maendeleo polepole au haraka kwa njia mpya. Je! Tunaweza kutumia muda gani uliowekwa wakfu kwa biashara, kwa raha, au kwa njia moja au nyingine? Je! Ni kiasi gani ya pesa zilizowekwa wakfu tutawezakutumia sisi wenyewe? Yote hayo yanapaswa kudhibitiwa na Agano letu na Mungu. Lazima tutafute kwanza mapenzi ya Bwana na Ufalme Wake. Hizi lazima ziwe za kwanza katika mipango yetu yote, ndipo mambo ya kidunia yawe ya pili. Kwa hivyo umuhimu wa tabia thabiti, nia sahihi na yasiyokwepa Mungu.

Mithali 16:32 *Asiye mwepesi* wa hasira ni bora kuliko mashujaa; na yeye atawalaye roho yake kuliko yule autwaye mji.